Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Kutawassal Kwa Mawalii Wa Mwenyezi Mungu

Mas-ala ya kutawassal Kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu na wapenzi wake ni mas-ala yanayofahamika miongoni mwa Waislamu ulimwenguni kote, na zimekuja hadithi nyingi kuruhusu jambo hili na kulipendekeza.

Kwa hiyo kutawassal siyo jambo geni bali ni jambo la kidini lililofahamika miongoni mwa Waislamu tangu mwanzoni mwa kuja Uislamu mpaka leo hii, na wala humkuti Muislamu anayelipinga.

Kwa muda wote wa karne kumi na nne tangu kuja Uislamu, hapana yeyote aliyelipinga jambo hili isipokuwa Ibn Taymiyyah na wanafunzi wake katika karne ya nane Hijiriya.
Na baada ya karne mbili akaja Muhammad bin Abdil-Wahab, ambaye yeye wakati mwingine akaona kuwa kutawassal kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu ni Bid'a na wakati mwingine akaona kuwa eti ni kuwaabudu Mawalii hao.

Hapana shaka yoyote kwamba kumuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu ni shirki na ni haramu.

Sisi sasa hivi hapa hatufanyi uchunguzi juu ya neno Ibada na uhakika wake ingawa jambo hili ni muhimu sana, lakini tutalizungumzia kwa ufafanuzi katika mahali pake maalum, kwa kuwa sasa hivi tunashughulika na kutawassal kwa Mawalii.

Hivyo basi tunasema: Fahamu (ewe msomaji) kwamba, kutawassal kwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu kuna namna mbili:

Kutawassal kwa Mawalii wao wenyewe nafsi zao kama vile tukisema: "Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nintawassal kwako kwa Mtume wako Muhammad [s] nikubalie haja yangu".

Kutawassal kwa cheo cha Mawalii na utukufu waliyonao mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kama vile tukisema:
"Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi ninatawassal kwako kwa utukufu wa Muhammad na heshima yake na haki yake unikubalie haja yamgu."

Kwa upande wa Mawahabi, wao wanaziharamisha namna zote mbili, wakati ambapo hadithi tukufu za

Mtume [s] na sera ya Waislamu vinashuhudia kinyume cha madai ya Kiwahabi na pia vinatilia mkazo kuwa namna zote mbili zinafaa.

Hivi sasa tunataja baadhi ya hadithi hizo moja baada ya nyingine, kisha tutaleta maelezo juu ya sera ya Waislamu, na hapo ndipo itakapoyeyuka na kupotea kauli ya mwenye kuharamisha tawassul na kuwa eti ni Bid'a.

Source URL:
https://www.al-islam.org/uchunguzi-juu-ya-uwahhabi-ayatullah-jafar-subhani/kutawassal-kwa-mawalii-wa-mwenyezi-mungu#comment-0